

(SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA YA 288)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89(1)

**SHERIA NDOGO ZA (UTAMADUNI NA VIBALI VYA BURUDANI) ZA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI ZA MWAKA 2019**

**SEHEMU YA I
MASHARTI YA AWALI**

- Jina la Sheria* 1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Utamaduni na Vibali vya Burudani) za Halmashauri ya Manispaa ya Lindi za Mwaka 2019
- Matumizi* 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.
- Tafsiri* 3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo tafsiri za maneno zitatumika kama ifuatavyo:-
- “Ada au ushuru wa kibali” maana yake ni tozo inayotozwa kwa Muombaji wa kibali cha burudani.
- “Afisa Mwidhiniwa” maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi wa Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.
- “Burudani” maana yake ni sherehe, shughuli, michezo yoyote inayokutanisha watu wawili au zaidi katika ukumbi, uwanja wa michezo, barabarani au sehemu yoyote ile bila kujali kama kuna matumizi ya sauti au la.
- “Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.
- “Kibali cha Burudani” maana yake ni ruhusa ya maandishi yenye

masharti inayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha sherehe, shughuli, michezo yoyote inayokutanisha watu zaidi ya wawili katika ukumbi, uwanja wa michezo, barabarani au sehemu yoyote ya wazi ambapo sauti ya juu itajitokeza.

“Matangazo” maana yake ni maandishi yoyote yaliyoandikwa, kubandikwa, kuchapishwa kwa namna yoyote ile ikiwepo kieletroniki yenye lengo la kutangaza au kuelezea biashara, shughuli, sherehe, tukio, elimu au sababu nyingine yoyote yenye nia ya kutengeneza mkusanyiko wa watu wanaoweza.

“Matangazo ya sauti” maana yake ni matangazo yanayotolewa kwa kutumia mdomo, vipaza sauti au chombo chochote kinachoweza kutoa sauti inayoweza kusikika kwa watu wengi.

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi au mtumishi yeyote atakayekuwa akikaimu nafasi hiyo.

SEHEMU YA II UTOAJI WA VIBALI VYA BURUDANI

Mamlaka ya Halmashauri kutoa vibali vya burudani na utamaduni

4. (1) Halmashauri itatoa vibali vya burudani kwa mtu yeyote, taasisi, shirika, kampuni, kikundi inayokusudia kufanya jambo lolote litakalotafsiriwa kuwa burudani chini ya Sheria Ndogo hizi au sheria nyingine yoyote ya nchi inayoipa Halmashauri uwezo huo.
- (2) Halmashauri itatoa vibali kwa waganga wa kienyeji na waganga wa tiba mbadala wote watakokuwa wakifanya shughuli katika eneo la Halmashauri. Kibali kwa mujibu wa Sheria hizi hakitatolewa kwa waganga wanaofanya ramri chonganishi au shughuli za kichawi.

Maombi ya kibali cha kufanya burudani

5. (1) Mtu yeyote mwenye nia ya kufanya jambo lolote litakalotafsiriwa chini ya Sheria Ndogo hizi kuwa burudani atapaswa kuomba kibali kwa njia ya maandishi na kulipia ada au ushuru kwa Mkurugenzi.
2. Malipo ya ada ya burudani yatalipwa kabla ya burudani husika kuanza kufanyika kwa viwango ambavyo vimeanishwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

3. Kibali cha burudani kitaonesha aina ya shughuli, mahali muda wa kuanza na kumaliza burudani na masharti ya kibali hicho na muombaji atalazimika kujaza fomu ya maombi kama ilivyo katika jedwali ya Tatu ya Sheria Ndogo hizi
- Wajibu wa kutii mamlaka zingine za Serikali** 6 (1) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 5 hapo juu muombaji wa kibali atawajibika kufuata utaratibu mwingine wowote uliomo katika sheria nyinginezo pamoja na maelekezo ya mamlaka nyingine za Serikali sawa na Mahitaji ya wakati husika.
- (2) Kibali kitakachotolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi hakitatafsiriwa kuwa ni ruhusa ya kuvunja sheria nyingine yoyote, hivyo iwapo mwenye kibali atavunja Sheria yoyote ya nchi atashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria hiyo.
- Vibali vya klabu za usiku au kasino** 7 Itakuwa ni kosa kwa mtu yoyote kufanya shughuli za klabu ya usiku au kasino bila kuwa kibali kutoka katika mamlaka husika.
- Masharti ya kibali cha burudani** 8 (1) Halmashauri itakuwa na haki ya kukataa kutoa kibali, kuzuia au kusitisha shughuli yoyote ya burudani ikiwa shughuli hiyo inavunja sheria za nchi, au kuchangia, kusababisha uharibifu wa maadili ya Mtanzania.
- (2) Burudani hazitaruhusiwa katika barabara ama maeneo yaliyo karibu na maeneo yote ya huduma za kijamii pamoja na maeneo ya ibada, mashule, na maeneo yote yenye ofisi za umma. Halmashauri inaweza kutoa kibali kufanyika kwa burudani katika maeneo hayo iwapo kwa maoni ya Mkurugenzi au Afisa mwidhiniwa inafaa kufanyika hivyo na kwa usimamizi maalum.
- Muda wa matangazo ya sauti** 9 Isipokuwa kwa kibali maalum toka Halmashauri na isipokuwa matangazo ya Serikali, matangazo yanayotumia vipaza sauti yataruhusiwa kuanza saa saba mchana hadi saa kumi na mbili jioni.
- Burudani za watoto** 10 (1) Sheria hii haitaondoa haki ya mtoto kupata burudani na kuongeza kipaji chake kadri awezavyo.
- (2) Burudani za watoto hazitafanyika katika maeneo au karibu na

maeneo zinapouzwa pombe na vinywaji vingine vya kulevya. Itakuwa ni marufuku kwa burudani za watoto kufanyika katika klabu ya usiku au kasino.

- (3) Burudani za watoto kama disko toto zitafanyika baada ya kupata kibali cha Halmashauri katika ukumbi:
 - a. wenye eneo kubwa la kutosha na hewa safi kadri itakavyotafsiriwa na Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa;
 - b. wenye eneo lisilokuwa na michoro, picha, video zinazokiuka utamaduni wa Mtanzania;
 - c. eneo lisilokuwa na wahudumu wanaovaa mavazi yanayoonyesha maungo yao na ambayo kwa maoni ya Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa yanakiuka maadili ya Mtanzania;
 - d. ambao upo karibu na maeneo zinapouzwa pombe au vileo vingine au katika klabu ya usiku au kasino;
 - e. ambao nyimbo na michezo inayochezwa haikiuki maadili ya Mtanzania.
4. Shughuli yoyote ya burudani itakayofanyika kuanzia saa kumi na mbili jioni au itakayozidi saa kumi na mbili jioni haitawahusisha watoto.
5. Mmiliki wa eneo, mpangaji anayefanya biashara au mtu mwingine yoyote atakayehusika kukiuka masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa.

SEHEMU YA III

MAKOSA NA ADHABU

- | | | |
|------------------------------------|----|---|
| <i>Mamlaka ya Afisa mwidhiniwa</i> | 11 | <ol style="list-style-type: none">(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na haki ya kuingia na kukagua eneo lolote linaloombewa kibali cha burudani wakati wowote na kutoa maelekezo kuhusu namna ambavyo burudani inayoombewa kibali au kukagua ikiwa burudani inayoendelea inazingatia masharti ya kibali.(2) Mtu yoyote atakayemzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa. |
|------------------------------------|----|---|

- Makosa** 12 (1) Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote:-
- a. Kuendesha shughuli ya burudani bila kupata kibali cha Mkurugenzi;
 - b. Kukataa au kushindwa kutii maagizo halali ya Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa;
 - c. Kumzuia kwa namna yoyote ile Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake;
 - d. Kukataa au kujaribu kukataa kulipa ada anayopaswa kulipa
 - e. Kushawishi mtu au kundi la watu kutolipa ada au ushuru;
 - f. Kuleta fujo au vurugu katika eneo lilipewa kibali cha burudani;
 - g. Kwenda kinyume cha mojawapo ya vifungu vya Sheria Ndogo hizi
- Adhabu ya jumla** 13 Mtu yeyote atakayetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi na akatiwa hatiani kama hakuna adhabu mahsusi iliyotajwa atatakiwa kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au vyote kwa pamoja faini na kifungo.
- Kufifilisha kosa** 14 Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (50,000) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kama iliyoelekezwa katika jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi

JEDWALI LA KWANZA
ADA YA VIBALI VYA BURUDANI
[Limetungwa chini ya kifungu cha 5(2)]

Na.	Aina ya kibali	Ada ya kibali Tsh.
1.	Dansi kutoka nje ya mkoa	50,000/= kwa siku
2.	Taarab na bendi kutoka nje ya Mkoa	50,000/= kwa siku
3.	Sherehe za Harusi	30,000/= kwa siku
4.	Disco/Dansi/Taarabu vikundi ndani ya Halmashauri	20,000/= kwa siku
5.	Sherehe za Camp za Vijana	20,000/= kwa siku
6.	Road Show na Promotion	50,000/= kwa siku
	Promotion za kuuza dawa za tiba asili	30,000/= kwa siku
7.	kurikodi Filamu na Harusi katika Bustani na maeneo ya wazi na Kumbukumbu	20,000/= kwa siku
8.	Matambara ya Burudani (Banners) yanayofungwa katika maeneo mbalimbali ndani ya	15,000/= kwa siku saba
9.	Matangazo madogomadogo (Posture) katika nguzo, miti, kuta mbalimbali	10,000/= kwa siku saba kwa posture
10.	Matamasha	50,000/= kwa siku
11.	Ngoma za Asili	10,000/= kwa siku
12.	Sherehe/tamasha/tafrija zingine zisizoorodheshwa humu	30,000/= kwa siku
13.	Kukodi eneo ya kufanyia burudai (Fukwe)	50,000/= kwa siku
14.	Kufunga barab	30,000/= kwa siku

JEDWALI LA PILI
FOMU YA KUFIFILISHA KOSA
(Limetungwa chini ya kifungu cha 14)

Mimi wa
SLP..... niliyeomba kibali/nilifanya burudani aina ya
..... katika eneo la
..... lililopo ndani ya Halmashauri ya Manispaa
ya Lindi nakiri kuwa leo tarehe nilikiuka kifungu cha
..... cha Sheria Ndogo za (Utamaduni na Vibali vya Burudani) za
Halmashauri ya Manispaa ya Lindi za mwaka 2019. Kwa hiyo, kwa hiari
yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa kiasi
cha ushuru ninachodaiwa pamoja na faini iliyoainishwa kwenye Sheria
Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya
kifungu cha 14 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini

Jina

Mbele yangu

Saini

Wadhifa

JEDWALI LA TATU
FOMU YA MAOMBI YA KIBALI
(Limetungwa chini ya kifungu cha 5(3))

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALAZA MIKOA NA SERIKALIZA MITAA
Halmashauri ya Manispaa ya Lindi

Telegraphic address
Tel: 023-220-2164
Fax: 023-220-2116
E-mail: lindimc.lindi@gg.tz



Ukumbi wa Manispaa,
S.L.P 1070,
LINDI.

Kumb. Na. LMC/.....

Tarehe

YAH: KIBALI CHA

Idara ya Elimu Kitengo cha Utamaduni Halmashauri ya Manispaa ya Lindi
inatoa kibali kwa;

Ndugu/Kikundi/Jumuiya/Idara/Shirika

Kutoka Wilaya ya Mkoa wa

Kata ya Kufanya

Katika Ukumbi wa/eneo la Nyumba Na. Mtaa wa

Tarehe Kuanzia saa Hadi saa

.....
Sahihi ya Mtoa Kibali

Idhini ya Afisa Utamaduni

Maoni ya Afisa Afya/Mazingira

Maoni ya Mkuu wa Kituo cha Polisi

MWEKA HAZINA

Malipo ya Kibali Tsh.

Sahihi Tsh

JUMLA

Nembo na mhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuata azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 28 mwezi Januari, 2019.

.....
Jomaary M. Satura,
Mkurugenzi,
Halmashauri ya Manispaa Lindi

.....
Mohamed L. Lihumbo
Mstahiki Meya,
Halmashauri ya Manispaa Lindi

NAKUBALI:

.....
Suleimani S. Jafo (MB),
WAZIRI OR - TAMISEMI

DODOMA
Tarehe/.....2019

